GAZETI RASMI LA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

(Hupigwa Chapa kwa Amri ya Serikali)

Sehemu ya CXXIV Nam. 6551 **13 Februari, 2015** **Bei Shs. 2500/=**

Imekubaliwa na Mkuu wa Posta kuwa ni Gazeti *Hutolewa kila Ijumaa*

YALIYOMO *Ukurasa*

Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Nam. 2 ya mwaka 2005.

Kanuni za Mafao ya Uzazi kwa wanachama wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar za mwaka 2014.
(Chini ya Kifungu cha 44(1)(b))..... 19

SEHEMU YA SHERIA

Tangazo la Sheria lililotajwa hapo chini limetangazwa katika ***Gazeti Rasmi*** hili.

Tangazo la Sheria

Nam. 31:- Kanuni ya Mfuko wa Hifadhi.

TANGAZO NAM. 30

SHERIA YA MFUKO WA HIFADHI YA JAMII NAM. 2 YA MWAKA 2005

KANUNI YA MAFAO YA UZAZI KWA MWANACHAMA WA MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR ZA MWAKA 2014.
(Chini ya kifungu cha 44 (1)(b))

KWA UWEZO niliopewa chini ya Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar, Nam. 2 ya Mwaka 2005, **MIMI OMAR YUSSUF MZEE,** Waziri wa Fedha, Zanzibarn natunga Kanuni zifuatazo:-

SEHEMU YA KWANZA
UTANGULIZI

1. Kanuni hizi zitajulikana kuwa ni Kanuni za Mafao ya Uzazi kwa wanachama wa Mfuko wa Hifadhii ya Jamii Zanzibar 2014, na zitaanza kutumika mara baada ya kuweka saini na Waziri na kuchapishwa katika Gazeti Rasmi la Serikali. Jina fupi na kuanza kutumika.

Matangazo yaliyohusu maiti, kuvunjikia kwa Ushirika na baadhi ya matangazo ambayo ni muhimu kwa watu kujua yanaweza kutiwa katika Gazeti. Nakala matangazo namna hiyo, zipelekwe kwa Mhariri wa Gazeti Rasmi la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar - Tanzania katika nyumba ya kupiga Chapa, Sanduku la Posta 261. Nakla zisichelewe kuliko Jumatatu kila wiki.

Kusomwa.

2. Kanuni hizi zitasomwa na zitatumika pamoja na Kanuni za Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar, Tangazo la Serikali Nam. 107 la 2007 ambazo katika Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni Kuu.

Ufafanuzi

3. Katika Kanuni hizi,]isipokuwa itakavyoeleza vinginevyo.

"Bodi" maana yake ni Bodi ya Wadhamini ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar iliyoanzishwa katika kifungu cha 6 cha sheria;

"Daktari anaetambulika" maana yake ni daktari aliesajiliwa chini ya Sheria ya Madaktari, Zanzibar;

"Hospitali inayotambulika" maana yake ni hospitali ya umma, vituo vya afya, zahanati zinazotoa huduma za uzazi au Hospitali Binafsi iliyosajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Hospitali binafsi, Zanzibar na haijumuishi maduka ya dawa;

"Kanuni Kuu" maanayake ni Kanuni za Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar, zilizotangazwa katika toleo la CXVI Nam. 6226, Tangazo la Serikali Nam. 107 la 2007.

"Kujifungua"maana yake ni hali ya mwanachama kupata mtoto baada ya kufikia wiki ya ishirini na nane (28) ya ujauzito akiwa hai au amekufa baada ya kuthibitishwa na daktari anayetambulika;

"Mafao ya Uzazi"maana yake ni kiwango maalum cha malipo ya fedha taslimu yanayolipwa kwa mwanachama mwanamke wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar kwa mujibu wa masharti na taratibu zilizoelezwa katika kanuni hizi;

"Mapacha"maana yake ni watoto wawili au zaidi;

"Mwanachama"maana yake ni mwanachama mwanamke wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar;

"Mfuko"maana yake ni Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar;

"Mkurugenzi Mwendeshaji"maana yake ni Mkurugenzi Mwendeshaji wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 14 sheria;

"Ujauzito" maana yake ni hali ya mwanachama mwanamke kuwa na mimba iliyofikia wiki ya ishirini na nane (28) tokea kupatikana kwa mimba hiyo;

"Msaada wa mafao ya uzazi kwa mwanachama aliyejifungua watoto mapacha" maana yake ni mafao ya ziada kwa mtu aliyejifungua mapacha;

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar, Nam.2 ya mwaka 2005;

"Waziri" maana yake ni waziri anaehusika na mambo ya fedha kwa wakati huu.

SEHEMU YA PILI
STAHILI NA TARATIBU ZA MAOMBI YA MAFAO YA UZAZI

Kustahili Mafao ya Uzazi

4.-(1) Kila mwanachama mwanamke atastahili kulipwa mafao ya uzazi kutoka Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar baada ya kutimiza sifa na masharti yaliyowekwa katika kanuni hizi.

(2) Mafao ya uzazi yatalipwa kwa mwanachama kila baada ya kipindi cha miaka mitatu kutoka kipindi mwanachama alicholipwa malipo ya mwisho ya mafao ya uzazi isipokuwa:-

(a) iwapo mwanachama atajifungua na mtoto wake kufariki ndani ya kipindi cha miezi sita (6) ya mwanzo kutoka siku aliyojifungua, au

(b) iwapo mwanachama atajifungua mtoto ambae amefariki akiwa tumboni.

Sifa za kulipwa Mafao ya Uzazi

5.-(1) Mwanachama atastahili kulipwa mafao ya uzazi baada ya kutimiza sifa zifuatazo:-

(a) mwanachama mwanamke aliyesajiliwa katika Mfuko kuwa mwanachama mnufaika;

(b) amechangia asilimia moja (1) ya mshahara wake katika Mfuko kwa kipindi kisichopungua miezi thelathini na sita (36) kabla ya kujifungua au kabla ya kuomba mafao; au

(c) amechangia michango ya miezi 36 kabla ya kujifungua au kabla ya kuomba mafao.

Isipokuwa kwamba miezi sita (6) katika miezi 36 au michango ya miezi thelathini na sita (36) iwe imechangiwa mfululizo karibu na wiki ya kujifungua au baada ya kujifungua.

(2) Katika kuthibitisha kuwa mwanachama amechangia asilimia moja (1) ya mshahara wake, Mfuko utazingatia mgawanyo wa asilimia iliyotajwa katika Sheria kuhusu mchango wa mwanachama uliowasilishwa katika Mfuko kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 1(2) (a) na (b) cha Jadweli la Kwanza la Sheria.

(3) Bila ya kuathiri masharti ya kanuni ya 5(1)(c) ya kanuni hii mwanachama ambae atakuwa anaomba mafao ya uzazi akiwa amejifungua mtoto wa pili na kuendelea atapaswa kulipwa mafao hayo iwapo atakuwa amechangia miezi ishirini na nne (24) au michango ya miezi ishirini na nne (24) kutoka mara ya mwisho alipolipwa mafao ya uzazi.

Jinsi ya Mafao ya Uzazi yakavyolipwa

6.-(1) Mwanachama atakaetimiza sifa na masharti yaliyoelezwa katika kanuni hizi atalipwa mafao ya uzazi ikiwa ni fedha taslim.

(2) Mfuko unaweza kuanzisha na kulipa mafao ya uzazi katika mfumo mwingine usiokuwa wa fedha taslimu kwa kadri utakavyoona kuwa inafaa kulingana na uwezo wa Mfuko kwa wakati huo baada ya kufanya tathmini ya uhai wa Mfuko.

(3) Malipo ya Mafao ya Uzazi yatalipwa kwa mwanachama kwa njia ya hundi au moja kwa moja katika hesabu ya benki ya mwanachama au kwa njia nyingine yoyote ambayo Mkurugenzi Mwendeshaji ataona inafaa

Kiwango cha Mafao ya Uzazi kinacho lipwa

7. Mfuko utalipa mafao ya uzazi kwa mwanachama kwa mujibu wa fomula iliyowekwa katika Jadweli la Kwanza la Kanuni hizi.

Muda wa Malipo ya Mafao ya Uzazi

8.-(1) Malipo ya Mafao ya Uzazi yatalipwa kwa awamu moja (1) iwapo yataombwa baada ya kujifungua na yatalipwa kwa awamu mbili (2) iwapo yataombwa kabla ya kujifungua.

(2) Mfuko utafanya malipo ya mafao ya uzazi baada ya mwanachama kukamilisha taratibu za maombi zilizoelezwa katika Kanuni hizi.

(3) Mwanachama ambae atajifungua mtoto ambae amefariki akiwa tumboni atastahili kulipwa awamu moja tu ya malipo ya mafao ya uzazi.

(4) Mwanachama ambae ataomba malipo ya mafao ya uzazi kabla ya kujifungua atapaswa kuomba mafao hayo katika kipindi kisichokuwa chini ya wiki ya ishirini na nane (28) tokea alipopata ujauzito.

(5) Malipo ya mafao ya uzazi baada ya kujifungua yatalipwa ndani ya kipindi cha siku tisini (90) baada ya mwanachama kujifungua.

Kutostahili kulipwa Mafao ya Uzazi

9.-(1) Bila ya kuathiri masharti ya kanuni ya 4(1) ya Kanuni hizi mwanachama hatostahili kulipwa mafao ya uzazi iwapo:-

(a) hajatimiza miezi thelathini na sita (36) ikiwemo miezi sita (6) mfululizo ya kuchangia katika Mfuko kutoka tarehe aliyoanza kuchangia na tarehe anayoomba mafao ya uzazi au tarehe aliyojifungua;

(b) atajifungua kwa kipindi kisichofikia miaka mitatu (3) kutoka tarehe ya mwisho aliyolipwa mafao ya uzazi isipokuwa iwapo atathibitisha kutokea mojawapo ya mambo yaliyoainishwa katika kanuni ya 4(2) (a) na (b);

(c) ataomba mafao ya uzazi kabla ya kujifungua chini ya kipindi cha wiki ya ishirini na nane (28) tokea alipopata ujauzito;

(d) hajatimiza miezi ishirini na nne(24)ya kuchangia au michango ya miezi ishirini na nne(24) iwapo mwanachama atakuwa anaomba mafao ya uzazi kwa kujifungua mtoto wa pili na kuendelea; au

(e) iwapo atawasilisha maombi ya mafao ya uzazi baada ya siku tisini (90) baada ya kujifungua.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kanuni ya 9(1) (e) Mkurugenzi Mwendeshaji anaweza kupokea na kukubali kufanyika malipo ya mafao ya uzazi kwa mwanachama baada ya kupindukia muda wa siku tisini (90) baada ya kujifungua iwapo mwanachama ataonesha sababu za msingi zilizosababisha kuchelewa kufanya maombi ya mafao ya uzazi na ambapo Mkurugenzi Mwendeshaji ataridhika na sababu hizo.

10.-(1) Mwanachama atawasilisha maombi ya mafao ya uzazi kabla ya kujifungua au baada ya kujifungua kwa kujaza fomu maalum ya maombi ya mafao ya uzazi kama ilivyoelezwa katika Jadweli la Pili la Kanuni hizi. Utaratibu wa maoni ya Mafao ya Uzazi

(2) mwananachama atawasilisha fomu ya maombi ya mafao ya uzazi iliyojazwa kwa ukamilifu pamoja na hati zifuatazo:-

(i) Barua ya maombi ya mafao ya uzazi.

(ii) Kadi ya Uanachama wa Mfuko.

(iii) Uthibitisho wa Daktari anaetambulika kuthibitisha tarehe anayotarajia kujifungua au tarehe aliyojifungua.

(iv) Kivuli cha gamba la kliniki la muombaji.

(iii) Kivuli cha gamba la kliniki la mtoto.

(iv) Nakala ya barua ya likizo ya uzazi kutoka kwa mwajiri

(v) Picha moja ya aina ya pasi ya kusafiria.

(vi) Hati nyingine zozote zinazoweza kuthibitisha maombi hayo.

(3) Bila ya kuathiri masharti ya Kanuni ya 10(2) na (3) ya Kanuni hizi, Mkurugenzi Mwendeshaji anaweza kupokea na kukubali hati au ushahidi mwingine wowote unaotilia nguvu maombi ya mafao ya uzazi iwapo, baada ya kushauriana na Daktari anaetambulika, ataona kuwa unafaa.

SEHEMU YA TATU
MENGINEYO

11. Hakutakuwa na malipo ya mafao ya uzazi kwa mwanachama ambae atajifungua na kufariki wakati wa kujifungua. Malipo ya Mafao kwa mwanachama aliyefariki wakati wa kujifungua

12.-(1) Mfuko utatoa malipo ya ziada ya mafao ya uzazi kwa mwanachama ambae atajifungua watoto mapacha baada ya kupata mafao ya uzazi ya kawaida ambayo anastahili. Msaada wa Mafao ya ya Uzazi kwa mwanachama aliyejifungua watoto mapacha

(2) Malipo ya ziada kwa kujifungua watoto mapacha yatakuwa nusu ya malipo ya mafao ya uzazi ya awamu moja.

(3) Malipo ya ziada ya mafao ya uzazi kwa kujifungua watoto mapacha yatalipwa mara moja tu katika awamu ya pili.

13.-(1) Bodi kwa kushauriana na Waziri inaweza kuongeza au kupunguza viwango vya malipo ya mafao ya uzazi kwa kadri itakavyoona inafaa. Mamlaka ya Waziri kuongeza au kupunfuza viwango vya mafao ya Uzazi

(2) Katika kutekeleza mamlaka yaliyoainishwa katika Kanuni ya 13(1) ya Kanuni hizi, Waziri atazingatia uwezo wa Mfuko kwa wakati huo na hali halisi ya uhai wa Mfuko kutokana na Ripoti za Tathmini ya Uhai wa Mfuko zinazofanywa kila baada kipindi cha miaka mitatu.

14. Bodi kwa kushauriana na Waziri itapitia na kuweka fomula ya uzazi kila baada ya kipindi cha miaka mitatu. Malipo ya Fomula ya malipo ya Uzazi

Kufutwa kwa Kanuni ya 23(6) ya Kanuni Kuu, 2007

15. Kanuni ya 23(6) ya Kanuni Kuu inafutwa.

JADUWELI LA KWANZA
FOMULA YA MAFAO YA UZAZI

Fomula ya Mahesabu ya Mafao ya Uzazi

1.-(1) Mafao ya uzazi yatakokotolewa kama ifuatavyo:-

(a) Wastani wa mshahara wa mwezi wa wanachama wote wa Mfuko kwa mwezi x 0.3.

(2)Mfuko utatangaza kiwango cha wastani wa mshahara utakaotumika kukokotoa mafao ya uzazi kila baada ya kipindi cha miaka mitatu.

JADWELI LA PILI
MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR
S.LP 2716
ZANZIBAR.

FOMU YA MAOMBI YA MAFAO YA UZAZI

(Tafadhali soma kwa uangalifu kabla ya kujaza fomu hii na tumia herufi kubwa tu). Fomu hii ijazwe mbele ya Afisa wa ZSSF.

MAELEZO.

1. Fomu hii itatolewa bila ya malipo.
2. Fomu hii ni lazima ijazwe na mwanachama ambaye ni mja mzito anatarajia kujifungua au mwanachama ambae ameshajifungua.
3. Fomu hii ijazwe si chini ya wiki ya ishirini na sita kutoka siku mwombaji alipopata ujauzito.
4. Mwombaji ni lazima ajaze majina ambayo yanaowana na majina yaliyomo katika kadi ya uanachama.
5. Mwombaji ni lazima aambatanishe na kadi ya uanachama pamoja na barua ya maombi ya mafao ya uzazi, kadi ya uanachama wa Mfuko, Uthibitisho wa daktari anaetambulika kuthibitisha tarehe anayotarajia kujifungua au tarehe aliyojifungua, kivuli cha gamba la kliniki la mwombaji au kivuli cha gamba la kliniki la mtoto, nakala ya barua ya likizo ya uzazi kutoka kwa mwajiri na picha moja ya aina ya pasi ya kusafiria.
6. Alama za vidole gumba ni lazima zisimamiwe na Afisa anaehusika katika ofisi za ZSSF.
7. Fomu hii ijazwe nakala mbili.

KWA MATUMIZI YA OFISI:

Imepokelewa na kuangaliwa na.....

Saini .....Tarehe.....

MUHURI WA ZSSF

SEHEMU "A"

MAELEZO YA MWOMBAJI

1. Jina kamili la Mwombaji .....

2. Nambari ya Uanachama wa ZSSF.....

3.Anuani kamili ya Mwombaji na pahala anapoishi.....

.....

4. Nambari ya simu ya mkononi.....

5. Jina kamili la Mama mzazi wa Mwombaji.....

6. Barua pepe ya Mwombaji.....

7. Tarehe uliyoajiriwa.....

8. Tarehe ya uliyojiunga na ZSSF.....

9. Tarehe unayotarajia kujifungua au tarehe uliojifunguwa.....

10. Naomba kulipwa mafao ya uzazi ninayostahiki kwa kuwa.....

(a) Natarajia kujifungua mnamo tarehe.....

(b) Nimejifunguwa mnamo tarehe.....

11. Iwapo umeshajifungua, jee mtoto yuko hai au amefariki?

(a) Mtoto yuko hai.....

(b) Mtoto amefariki.....

12. Umewahi kupata mafao ya uzazi kutoka ZSSF?

Ndio.....Hapana.....

13. Ikiwa ndio; eleza;

Kiwango ulicholipwa:	Tarehe uliyolipwa:

SEHEMU "B"
TAARIFA ZA AJIRA

Kazi unayofanya kwasasa: _____
Mwajiri wako wa sasa: _____
Anuani ya mwajiri wako wa sasa: _____
Iwapo umefanya kazi chini ya kipindi cha miaka mitatu kwa mwajiri wako wa sasa toa taarifa za waajiri wengine uliofanya kazi kama inavuooneshwa hapo chini.

Jina la Mwajiri	Anuani	Tarehe uliyoanza kazi	Tarehe ulioacha kazi

UTHIBITISHO WA MWAJIRI WA MWOMBAJI (kwa mwombaji ambaye bado yupo kazini)

Nathibitisha kwamba mwombaji ni mfanyakazi katika taasisi yangu na taarifa zote zilizoelezwa katika fomu hii ni za kweli. Mchango wake wa mwisho kabla ya mombi haya ulikuwa ni T.SH.....na zimelipwa ZSSF mnamo tarehe.....

Mwajiri.....
Anuani.....
Jina na cheo cha Afisa Muhusika
Saini .....

SEHEMU "C"
MALIPO YA MAFAO YA UZAZI.

Tamko la mwombaji kulipwa mafao ya uzazi moja kwa moja katika hesabu yake ya benki.

Natamka kuwa nimekubali kulipwa mafao ya uzazi kupitia hesabu yangu ya benki iliyoainishwa hapa chini:

Jina la Benki: _____
Tawi la Benki: _____

Nambari ya Hesabu: _____
Jina la mwenye Hesabu ya Benki: _____

Naambatanisha pamoja na (a) Cheti cha Kujifungua au (b) Cheti kinachoonesha tarehe ninayotarajia kujifungua. Nathibitisha kwamba maelezo yote niliyoyatoa katika fomu hii ni ya kweli na yananifunga kisheria..

Saini ya Mwombaji: _____ Tarehe: _____

Alama za Vidole gumba.....

Alama za vidole gumba zimethibitishwa na:-

Jina.....Saini.....Tarehe.....

MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR
CHETI CHA KUTHIBITISHA MATARAJIO YA KUJIFUNGUA

Fomu hii ijazwe na daktari anaetambulika tu na inatolewa kwa lengo la maombi ya mafao ya mafao ya uzazi tu kwa mwanachama aliyetajwa katika sehemu "A" hapo chini.

SEHEMU "A"
MAELEZO YA MWOMBAJI

1. Jina kamili la Mwombaji .....

2. Nambari ya Uanachama wa ZSSF.....

3. Anuani kamili ya Mwombaji .....

SEHEMU "B"
MAELEZO YA DAKTARI

Nathibitisha kwamba nimemchunguza_____ na kwamba ni mjamzito na anatarajia kujifungua mtoto mnamo tarehe.....

Jina la Daktari.....

Cheo.....

Nambari ya usajili ya Daktari.....

Saini _____ Tarehe ya Uchunguzi.

Muhuri

MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR
CHETI CHA KUTHIBITISHA KUJIFUNGUA

Fomu hii ijazwe na daktari anaetambulika tu na inatolewa kwa lengo la maombi ya mafao ya mafao ya uzazi tu kwa mwanachama aliyetajwa katika sehemu "A" hapo chini.

SEHEMU "A"
MAELEZO YA MWOMBAJI

1. Jina kamili la Mwombaji .....

2. Nambari ya Uanachama wa ZSSF.....

3. Anuani kamili ya Mwombaji .....

SEHEMU "B"
MAELEZO YA DAKTARI

Nathibitisha kwamba nimemchunguza _____ na nathibitisha

kuwa amejifungua mtoto mnamo tarehe.....

Jina la Daktari.....

Cheo.....

Nambari ya usajili ya Daktari.....

Saini _____ _____

Tarehe ya Uchunguzi.

Muhuri

Zimetiwa saini leo hii tarehe.....,....., 2014.

.....
(OMAR YUSSUF MZEE)
WAZIRI WA FEDHA
ZANZIBAR